# KIVUKO NA WATOTO

## MWONGOZO WA UNASIHI



Jovin F. Riziki
and Sue Holden

Practical Action Publishing Ltd
The Schumacher Centre, Bourton on Dunsmore, Rugby, Warwickshire, CV23 9QZ, UK
www.practicalactionpublishing.org

© The Salamander Trust, Jovin F. Riziki and Sue Holden. 2016

The rights of the authors to be identified as authors of the work have been asserted under sections 77 and 78 of the Copyright Designs and Patents Act 1988.

All rights reserved. Sections of the accompanying book to this guide listed in the Acknowledgements as under a Creative Commons licence may be reproduced without permission. No other part of this publication may be reprinted or reproduced or utilized in any form or by any electronic, mechanical, or other means, now known or hereafter invented, including photocopying and recording, or in any information storage or retrieval system, without the written permission of the publishers and Salamander Trust. However, if permission is sought and granted, extracts from the accompanying book to this guide may be reproduced for non-profit purposes, for example, for workshops organized by you or your organization, with acknowledgements to the author and the publisher. Permission may also be granted for adaptations or translations, but only in close communication with The Salamander Trust.

Product or corporate names may be trademarks or registered trademarks, and are used only for identification and explanation without intent to infringe.

Since 1974, Practical Action Publishing has published and disseminated books and information in support of international development work throughout the world. Practical Action Publishing is a trading name of Practical Action Publishing Ltd (Company Reg. No. 1159018), the wholly owned publishing company of Practical Action. Practical Action Publishing trades only in support of its parent charity objectives and any profits are covenanted back to Practical Action (Charity Reg. No. 247257, Group VAT Registration No. 880 9924 76).

The views and opinions in this publication are those of the author and do not represent those of Practical Action Publishing Ltd or its parent charity Practical Action. Reasonable efforts have been made to publish reliable data and information, but the authors and publisher cannot assume responsibility for the validity of all materials or for the consequences of their use.

Cover design by Mercer Design
Typeset by Bookcraft Ltd, Stroud, Gloucestershire
Printed by Replika Press, India

TUSAIDIANE PASADA

Salamander Trust
TRANSFORMING THE WAY WE THINK ABOUT HIV

# KIVUKO NA WATOTO:
# MWONGOZO WA UNASIHI KWA AJILI YA WATOTO WANAOISHI NA VVU NA WALIOATHIRIWA NA VVU NA WALEZI WAO

**Jovin F. Riziki na Sue Holden**


| | |
|---|---|
| Kuhusu Mwongozo huu wa Unasihi | 2 |
| Mambo ya msingi katika kuwanasihi watoto | 2 |
| Ni kitu gani cha tofauti katika kuwanasihi watoto? | 3 |
| Kurekebisha namna tunavyofanya kazi ili ifae kwa kila mtoto | 4 |
| Kufanya kazi na watoto na walezi wao | 6 |
| Kuwanasihi watoto kuhusu ujinsia | 8 |
| Kufuata taratibu za eneo na sheria kuhusiana na watoto | 8 |
| Usiri na maadili | 9 |
| Usiri | 9 |
| Taratibu za kimaadili wakati wa kuwanasihi watoto na walezi wao | 10 |
| Kuwanasihi watoto kwa ajili ya kipimo cha VVU | 10 |
| Unasihi kabla ya kupima | 11 |
| Unasihi baada ya kupima | 14 |
| Ushirikishaji wa hali ya uambukizo wa VVU wakati fulani baada ya kupima VVU | 16 |
| Unasihi wa mwendelezo kwa ajili ya watoto wanaoishi na VVU na walezi wao | 18 |
| Mara tu baada ya kushirikisha | 18 |
| Unasihi wa kuendelea | 18 |
| Kuwanasihi watoto kuhusu masuala maalum | 19 |
| Usiri na kushirikisha | 19 |
| Unasihi kuhusu Tiba ya Dawa za Kupunguza makali ya VVU (ARV) | 20 |
| Kuwanasihi watoto waliofanyiwa unyanyasaji wa kijinsia | 21 |
| Kuwanasihi watoto kuhusu kifo na kufariki | 23 |
| Maudhui ya mwisho | 25 |
| Vyanzo vya taarifa | 26 |

## Utambuzi

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa watu na mashirika tunaotambua kuwa walichangia katika mwongozo huu. Hapa Tanzania watu hawa wanajumuisha: Dr Theodor Tigawa kutoka Wizara ya Afya ba Ustawi wa Jamii; Dr Fausta Philip kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; na Elisius Mkolokoti, Josephine Daffi, Rose Kadesha, na Martha Kamuhabwa wa Pastoral Activities and Services for people with AIDS Dar es Salaam Archdiocese (PASADA). Kule UK ni: Silvia Petretti wa Positively UK; Dr Elspeth McAdam wa The Taos Institute; Kate Holden wa Time To Talk Counselling; na Gill Gordon na Alice Welbourn wa The Salamander Trust.

## Kuhusu mwongozo huu wa unasihi

Tumeandika mwongozo huu kwa ajili ya watu ambao tayari wana taarifa, na stadi, na uzoefu unaohitajika katika kuwanasihi watu wazima kuhusu VVU na masuala yanayohusiana. Hatujaweka taarifa za msingi, kama vile unasihi ni kitu gani au stadi za unasihi. Badala yake tumeweka mkazo katika taarifa zile za *nyongeza* na stadi ambazo wanasihi wanazihitaji ili wafanye kazi na watoto wa makundi yote mawili, wale walioathiriwa na VVU au wanaoishi na VVU, na walezi wao. Pia tumeainisha zile hatua muhimu za kufuata katika mazingira ya unasihi yanayojumuisha watoto na walezi.

Mwongozo huu umeambatanishwa na mitaala ya *Kivuko na Watoto*. Watoto na walezi ambao wanahudhuria warsha za *Kivuko na Watoto* hujifunza kuthamini uwezo wao, na kutafuta njia za kuzitumia katika kuboresha maisha yao. Kwa mfano: walezi kujifunza namna ya kuwafundisha watoto nidhamu badala ya kuwapiga au kuwaadhibu, wakati watoto wanajifunza namna ya kuweka mipaka kuhusiana na uhusiano wa kimapenzi (kingono), na namna ya kujikinga wao na wengine dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

> Wanasihi wanaweza pia kufaidika kutokana na kufanya mazoezi ya *Kivuko na Watoto*, kwa ajili ya uelewa wao binafsi na pia kwa ajili ya kuelewa zaidi masuala yanayowakabili walengwa wao. Kote ndani ya mwongozo huu – katika visanduku kama hiki – tutaweka bayana mazoezi ya kwenye mtaala wa *Kivuko na Watoto* ambayo mahususi ni ya usaidizi kwa wanasihi ili wayafanye wao wenyewe, au ambayo yanajumuisha taarifa za manufaa kwa ajili ya unasihi wao. Wanasihi mahiri ni lazima waupitie mtaala huo pamoja na kundi la wenzi wao, ili kuboresha taarifa zao ziwe za kisasa na kujizoesha katika mchakato mzima.

## Misingi ya kuwanasihi watoto

Unasihi kwa ajili ya watoto, kama vile kwa watu wazima, kunadhamiria kuwasaidia kuhimili mihemko na changamoto zinazohusiana na VVU na athari zake, na kufanya uchaguzi ambao utaboresha maisha yao katika misingi ya kuwa na uelewa. Japokuwa mkazo unaweza kuwa ni katika VVU, wanasihi wanahitaji kuona na kufanya kazi na mtoto huyo kwa ukamilifu wake: mambo yote yanayogusa maisha yake.

Kuwanasihi watoto hujumuisha:
✓ kuwasaidia wasimulie hadithi zao;
✓ kuwasikiliza kwa makini;
✓ kuwapatia taarifa sahihi na muafaka;
✓ kuwasaidia wafanye uamuzi utokanao na uelewa;
✓ kuwasaidia watambue na kujenga uimara wao;
✓ kuwasaidia kujenga mtazamo chanya katika maisha.

Kuwanasihi watoto haijumuishi:
- ✘ kufanya uamuzi kwa ajili yao;
- ✘ kuwahukumu au kuwalaumu;
- ✘ kuwahoji au kubishana nao;
- ✘ kuweka ahadi ambazo huwezi kuzitimiza;
- ✘ kuwahubiria au kuwafanyia mhadhara;
- ✘ kulazimisha imani zako kwao.

Majukumu yetu makuu wakati wa vipindi vya unasihi na watoto na walezi hujumuisha:
- Kuwasaidia waelewe hali zao na namna wanavyojisikia kwa kutafakari kile ambacho walitueleza hapo nyuma, kwa hali zote mbili; ya maneno na lugha ya mwili;
- Kuwasaidia kutafakari majuto yao na hisia za kujilaumu na hasira;
- Kuwasaidia ili waone wanachoweza kufanya ili kuboresha hali yao, hata kama mambo mengine yako nje ya udhibiti wao;
- Kuwasaidia kufanya uamuzi utokanao na uelewa;
- Kushirikishana nao taarifa zenye manufaa;
- Kuwasaidia katika kujenga ujasiri na kujiamini ili waweze kuibuka na mikakati yao wenyewe na matarajio na mipango kwa ajili ya hapo baadaye.

## Ni kitu gani cha tofauti katika kuwanasihi watoto?

Yapo mambo manne ya tofauti wakati tunawanasihi watoto kinyume na watu wazima.

1. Ni lazima turekebishe kile tunachokisema na kukifanya ili kishabihiane na umri na hatua za ukuaji wa kila mtoto. N lazima pawepo tofauti kubwa kati ya namna tunavyofanya kazi na watoto wa umri wa miaka mitano ambao wanaweza kuwa hawajajua kuandika bado, na wa umri wa miaka15 ambao wanaweza kuwa wamepevuka kimhemko.

2. Kwa kawaida huwa hatufanyi kazi na mteja mmoja-mmoja, bali na mtoto pamoja na mlezi (walezi) wake. Ni lazima tushughulikie matarajio na mahitaji yao mbalimbali, na kuwasaidia wafanye kazi pamoja.

3. Ni lazima tuwe tayari na uwezo wa kuongea na watoto kuhusu ngono na ujinsia, na tunaweza kuona ugumu katika mambo haya.

4. Tunahitaji kuwa makini kuhusu taratibu za maeneo na sheria ziwahusuzo watoto, kwa mfano, kujua ni katika umri gani na mazingira gani mtoto anaweza kufanya kipimo cha VVU bila ridhaa ya mlezi.

Hapa chini ni baadhi ya mawazo kuhusu namna ya kushughulikia tofauti hizo nne.

### Kurekebisha namna tunavyofanya kazi ili ishabihiane na watoto

#### *Kujenga mazingira rafiki*

Watoto wanahitaji wajisikie huru iwapo watawasiliana na sisi. Hapa kuna mambo unayoweza kuyafanya ili uweze kujenga hisia za mazingira rafiki kwa ajili ya vipindi vyako.
- Tabasamu!
- Vaa beji au mkufu wa shingoni ambao unawavutia watoto.
- Kuwa na wanasesere kadhaa na magazeti, ambayo ni muafaka kwa umri wa mtoto husika.

- Ondoa makaratasi na majalada.
- Weka ukutani picha zenye mvuto au mabango.
- Keti chini sakafuni ili kucheza na kupiga gumzo na wale watoto wadogo zaidi.

### *Kuwajumuisha watoto kama wateja*

Watoto wengi wanayo mazoea kwamba watu wazima wanawaambia kitu cha kufanya, kuwakosoa, na kutokuwasikiliza. Unahitaji kufanya kinyume cha hayo!

- Mwambie mtoto kipindi kitachukua muda gani.
- Tamka wazi ukaribisho, na ruhusu wajue kwamba wanaweza kucheza na kujipumzisha, kwa mfano 'Jambo, umekuja tena kucheza!' au 'Habari, ni wakati wa kupiga gumzo na Joshua!'
- Kwa wale watoto wadogo zaidi, anza kila kipindi kwa kucheza pamoja.
- Kwa wale wakubwa zaidi, anza kwa kupiga gumzo kuhusu kitu wanachokifurahia, kama vile soka, mziki, mtindo au sayansi.
- Pongeza na kusifia, kwa mfano 'Umeweka nguvu nyingi katika mtindo wako huo wa nywele' au 'Umefanya vizuri sana kufika hapa na mvua hii! Asante!'
- Usiharakishe; sikiliza kwa makini, na tambua kile mtoto akisemacho.
- Tumia lugha isiyo rasmi sana, isiyo na ya mafumbo, katika sentensi fupi. Rekebisha unachokisema ili kishabihiane na umri wa huyo mtoto na kiwango chake cha uelewa.
- Uwe mkweli.
- Sikiliza kuhusu uwezo wa mtoto, na uuweke bayana, kwa mfano 'Hiyo ilikuwa tabia ya ushujaa pale ambapo ulifanya hivyo! Unao ujasiri wa kufanya mambo magumu.'
- Uwe na mtazamo chanya, kwa mfano ongea kuhusu mana tunavyoweza kuishi vyema na VVU, badala ya kuweka taswira kwamba VVU ni ugonjwa unaositisha maisha.
- Toa taarifa iwapo inahitajika, katika njia ambayo mtoto anaweza kuelewa.
- Picha muafaka au wanasesere viwepo, ili vikusaidia kuelezea mawazo.
- Onesha kumfurahia huyo mtoto: kila mmoja ni wa namna ya pekee.
- Uwe na utayari wa kushughulikia mada na masuala yote, sio tu zile ambazo zinahusiana na VVU tu.

### *Kutumia mbinu mbalimbali kusaidia mawasiliano*

Wakati tunapowanasihi watu wazima tunategemea kuzungumza ili kuwasiliana. Kwa watoto, tunahitaji mikakati ya nyongeza. Mara kwa mara watoto wanaweza wasijue au kuweza kuongea kuhusu hisia zao. Wanaweza kuzificha hisia zao kwa sababu hawataki kuwaudhi walezi wao, au (kwa upande wa unyanyasaji) kumsababishia mtu fulani matatizo.

Mbinu zifuatazo zinaweza kuwa za msaada.

*Kuchora*. Watoto wengi hupenda kuchora, na kusifiwa kwa hiyo michoro yao. Iwapo utawataka wachore kitu fulani kinachohusiana na kitu unachotaka kukitafakari, unaweza kujifunza kutokana na kile watakacho-kichora na kukitumia kuzungumza nao. Usifanye chukulizi kuhusu michoro yao. Badala yake, tumia maswali ili kuwahamasisha waongee: kwa mfano 'ni nini kinatokea katika picha hii?' na 'mtu huyu anajisikiaje kuhusiana na kile kinachotokea?'

Iwapo mtoto akikubali, inaweza kuwa jambo la manufaa kwao kuwaonesha walezi picha zao, kwa majadiliano zaidi katika kile kipindi cha pamoja cha unasihi.

*Kusimulia hadithi*. Pale ambapo watoto wanaona ugumu kuongea kuhusu masuala yenye uchungu, kusikiliza hadithi kuhusu mtu fulani ambaye amekuwa katika mazingira kama hayo huweza kuleta faraja. Inaweza kuwapa fikra ya kuwa wameeleweka, na kuwasaidia kutambua kwamba hawako peke yao.

Hadithi inaweza kuchukua nafasi ya nyenzo ya kutatua tatizo kuzunguka mazingira fulani halisi ya mtoto. Simulizi za wahusika ambao wamezivuka hali ngumu katika maisha yao huwasaidia watoto wavute taswira ya kuvuka hali zao wenyewe zilizo ngumu.

Iwapo utatumia kusimulia hadithi, kwepa kutumia majina au matukio halisi. Pale mwishoni mwa hadithi mtie moyo mtoto aongee kuhusu kile kilichotokea, ili ujue kama amekielewa. Kisha, unaweza kutafakari husika ya hadithi hiyo katika maisha yao wenyewe.

Kumbuka kwamba huhitaji kuwa msimulia hadithi. Unaweza kuwasaidia watoto kuunda hadithi zao wenyewe, kutokana na mada unayowapatia, kwa mfano, ‘Nisimulie hadithi kuhusu msichana mdogo ambaye alikuwa mgonjwa lakini baadaye akapata nafuu.’

*Mchezo*. Kupatikana kwa wanasesere kwa ajili ya watoto kuchezea – kama vile visanduku vichache na mifano ya wanyama au binadamu – huwaruhusu waburudike. Unaweza kutaka kuweka umbo fulani katika mchezo wao kupitia njia ya kuwatafadhalisha kwa mfano ‘nioneshe siku ya furaha katika familia yako’. Kwa kuchunguza mchezo wao na kuuliza maswali ya wazi ni lazima ikusaidie kuelewa hisia zao, na kuweza kudhihirisha mahitaji na matatizo. Ungeweza pia kutumia michezo yao kutafakari uchaguzi, kwa mfano ‘ingetokea nini iwapo mhusika huyo hataki kwenda kliniki?’

> Iwapo watu unaowanasihi walikwisha kuwa kwenye warsha za *Kivuko na Watoto*, unaweza kutumia baadhi ya dhana hizo katika vipindi vyako, kama vile lile wazo la kurudi katika ‘habu yetu’ wakati tunajisikia kufadhaika (angalia Kipindi 2). Ungeweza pia kuwakumbusha watoto kuhusu yale mazoezi ya kupumua, na myafanye pamoja.

*Kuandika kuhusu uzoefu.* Watoto wenye umri mkubwa wanaweza kupenda kuandika mashairi, hadithi za kubuni, au simulizi za uzoefu wao wenyewe, ambavyo mnaweza kujadili pamoja baadaye. Kuwa na hakika kwamba mtoto ana furahia kuandika; kwa baadhi yao, ‘kazi ya shule’ kama hizo zinaweza kuwazuia kuja katika vipindi vya unasihi.

## Kufanya kazi na watoto na walezi wao

Mara nyingine, na iwapo inaruhusiwa, utamnasihi mtoto mkubwa ambaye hana msaada wa mlezi, hataki mlezi wake ahudhurie, au ambaye mlezi wake hatahudhuria au hawezi kuhudhuria. Katika hali kama hii utakuwa na kipindi na mtoto peke yake, rekebisha namna unavyofanya kazi ili ishabihiane na mtoto huyo. Iwapo mtoto huyo katika maisha yake hana mlezi mtu-mzima, itakuwa muhimu sana kumuunganisha na mitandao ya msaada.

Lakini, mara nyingi, watoto hufika kwa ajili unasihi wakiwa na mlezi. Au, iwapo unawatembelea nyumbani, wanaweza kuwepo wanafamilia wengine. Unaweza kutaka kufanya kazi na huyo mtoto na huyo mlezi tofauti-tofauti (iwapo unaruhusiwa), au kwa pamoja, au hali hizo zote mbili. Utahitaji kutumia busara yako kuamua ni hali ipi bora zaidi, kutegemea haiba za watu na mazingira katika kila suala. Hapa chini tunatoa mapendekezo ya jumla.

### *Ni wakati upi wa kufanya kazi na mtoto bila mlezi*

Unaweza kutaka kufanya kazi na mtoto mbali na kuwapo kwa mlezi iwapo:

- unaweza kutengeneza mahusiano wa kuaminiana na mtoto huyo, bila kuvurugwa na kuwapo kwa mlezi;
- unataka kung'amua masuala na hisia pamoja na huyu mtoto zenye uwezekano mdogo kwamba mtoto atataka zijadiliwe mbele ya huyo mlezi, kwa mfano, namna ambavyo mtoto anajisikia kuhusu mlezi huyo, pengine mtoto amenyanyaswa, na mada nyingine binafsi (kama vile maisha yao ya ngono);
- mlezi anayo hali ya kuingilia kati mawasiliano na mtoto, kwa mfano, kuongea kwa niaba ya mtoto, au kutawala mchezo wa huyo mtoto;
- kuwapo kwa mlezi kunaelekea kumzuia asiwasiliane na wewe, kwa mfano, mtoto anamwangalia mlezi ili kupata idhini ya kuongea, na kuonekana kuongea kile ambacho 'anaruhusiwa' kusema, badala ya kile anachotaka kusema.

Kutegemeana na taratibu zilizopo nchini mwenu na katika shirika lenu, unaweza kuhitaji awepo mtu mzima mwingine (kwa mfano nesi) wakati ule ambapo yule mlezi hayupo humo chumbani.

### *Ni wakati gani wa kufanya kazi na mlezi bila mtoto*

Unaweza kutaka kufanya kazi na mlezi mbali na kuwapo kwa mtoto:

- unataka kuchunguza masuala na fulani-fulani na mlezi, kwa mfano, hofu zao kuhusu huyo mtoto, au mada nyingine ambazo mlezi huyo hawezi kuziongelea kwa ukweli wakati mtoto akiwa anasikiliza;
- mtoto anavuruga, kwa mfano anasumbua, anahitaji kuangaliwa.

### *Ni wakati gani wa kufanya kazi na mtoto na mlezi kwa pamoja*

Unaweza kutaka kufanya kazi na wote wawili; mtoto na mlezi papo kwa papo:

- unapotaka kuwezesha majadiliano na utatuzi wa matatizo miongoni mwao;
- unapotaka kushirikisha taarifa fulani kwa wote wawili, mtoto na mlezi;
- mtoto anapo kuwa na hofu kuhusu kitu fulani, au haridhiki kuwa na wewe peke yenu.

### *Madokezo*

- Unapofanya kazi na mtoto au mlezi pekee, unaweza kumpatia kazi yenye manufaa huyo mwingine wakati anasubiri. Kwa mfano, mwambie achore picha, aandae hadithi, aandike namna anavyojisikia, aandae ramani ya kiakili, au asome taarifa fulani. Unaweza kudadisi kile walichofanikisha au kujifunza kipindi utakapokutana naye hapo baadaye.
- Iwapo mlezi anasita kukuruhusu uongee na mtoto peke yake, eleza kwamba ni jambo la kawaida na la manufaa kuwapatia fursa ya kuwa peke yao na mnasihi. Kwa upole na ubunifu mtafadhalishe amruhusu mtoto aitumie fursa hii. Iwapo bado anakataa, chunguza kujua ni kwa nini. Wanaogopa kitu gani? Pengine ingesaidia iwapo angekuwapo mtu mzima mwingine ndani ya hicho chumba? Eleza kwamba yapo masuala ambayo ungependa kuyadadisi na mtoto, kwa faida yao, na kwamba hapo baadaye utamjulisha mlezi mambo yaliyojiri.
- Wakati wa kufanya kazi na mtoto peke yake, hakikisha kwamba huyo mtoto anajua mlezi wake alipo, na sehemu hiyo ya kipindi hicho cha peke yenu kitakuwa ni muda gani.

### Unasihi kuhusu ujinsia

Kama mnasihi, tumezoea kujadili masuala ya ujinsia na watu wazima ila tunaweza kuhangaika sana kufanya hivyo na watoto. Hapa kuna baadhi ya mambo kwa ajili yako kuyafikiria, ili kuboresha uwezo wako wa kuwanasihi watoto kuhusu ujinsia.

*Uwe na tahadhari kuhusu uchaguzi na imani zako binafsi, na uweze kuziweka kando*. Hakuna mtoto anayetakiwa kujisikia kuhukumiwa na wewe, kwa mfano, iwapo atakuambia ameshafanya kitu ambacho wewe unajisikia kimaadili ni makosa kabisa, kama vile kufanya ngono au kujisikia kuvutiwa na mtu wa jinsi kama yake.

*Kumbuka kwamba ngono na ujinsia si 'masuala ya watu wazima'.* Tamaduni zetu zinaweza kutukatisha tamaa kuongea na watoto kuhusu ngono na ujinsia, lakini binadamu wote ni viumbe watokanao na ujinsia. Kuongea na watoto kuhusu ngono haiwasababishii wao kufanya ngono; badala yake huwafanya wajuzi zaidi ili kufanya uamuzi mzuri zaidi.

*Kupunguza kudhaliliswa.* Tafuta na jizoeshe kusema maneno na misemo muafaka kuendana na umri wa watoto wakati wa unasihi kuhusiana na ujinsia. Pia, kuwa na utayari kutumia misamiati wanayoitumia. Wateja watakuwa hawapati kizuizi au kujisikia kudhalilishwa iwapo wewe ni mtulivu na unajiamini.

*Uwe na mfumo wako wewe mwenyewe wa msaada.* Hakikisha kwamba unapata msaada wa kitaaluma kutoka kwa msimamizi au mshauri wako au kukusaidia kuhimili, usiri, kuhusiana na masuala ya kihisia ambayo yanaweza kujitokeza, kwa mfano wakati unamnasihi mtoto ambaye amenyanyaswa.

> Kipindi 21 ni kuhusu mambo yote yahusuyo hisia za kimapenzi na usalama wa kijinsia. Kitakusaidia wewe kuongea nao kuhusu mambo haya.

### Kufuata taratibu na sheria kuhusiana na watoto

Sheria zilizoandikwa zinatofautiana kutoka nchi hadi nchi, kama inavyokuwa katika namna ile sheria zinavyotafsiriwa kiutendaji. Shirika lako ni lazima lina taratibu zilizoandikwa ili kuwaongoza wanasihi wake, zikiainisha taratibu kuu na mpangilio wa utendaji kama hizi zifuatazo.

#### *Ridhaa*

- Umri ambao watoto wanahitaji ridhaa ya wazazi ili kufanya unasihi kwa ajili ya kipimo cha VVU.
- Taratibu za namna ya kueleza masuala ya ridhaa kwa watoto na walezi, na namna ambavyo unapima iwapo ridhaa imetolewa au kukataliwa.
- Tofauti na hizo taratibu za ridhaa ya wazazi, kwa mfano kwa ajili ya watoto wa mitaani, wale ambao wamefanyiwa ukatili wa kijinsia, na 'watoto wa chini ya miaka kumi na minane'.

#### *Usiri*

- Sheria zinazohusiana na usiri, na taratibu za kuhakikisha kuwapo kwa usiri.
- Taratibu za namna ya kujadili na kufanya makubaliano kuhusu usiri kwa watoto na walezi wao.
- Taratibu kuhusu haki za watoto kujua hali zao za maambukizo ya VVU ukilinganisha na matakwa ya walezi kuzuia kuwajulisha matokeo hayo.
- Tofauti na taratibu kuhusu usiri, kwa mfano kwamba hii itakiukwa kwa dharura ya kitabibu iwapo wafanyakazi wa afya wanahitaji kujua mtoto huyu anatumia tiba gani.

### *Ngono na unyanyasaji wa kijinsia kinyume na sheria*

- Umri ambao kisheria mtoto anaweza kufanya ngono ya mke na mume.
- Sheria zinazohusiana na ngono ya jinsi moja.
- Sheria na taratibu za kufuata kuhusiana na unyanyasaji.
- Sheria zinazohusiana na maambukizo ya VVU kupitia ngono.

## Usiri na maadili

Sehemu hii inatoa maudhui ya jumla ambayo sisi, tunahitaji kuyafuata kuhusu usiri na maadili, tunapowanasihi watoto.

### Usiri

Sisi sote tunayo haki ya usiri. Kufanya kazi kama wanasihi wa VVU, ipo hatari kwamba tunapumzisha fikra zetu kuhusu mambo haya, tukidhania kwamba hali ya maambukizo ya mteja wetu inajulikana kwa upana kwa sababu amekuja kwenye huduma zetu za VVU. Hatutakiwi kuingia katika mtego huu. Katika kila hatua tunahitajika kujihadhari na kuweka usiri, na kujadili usiri huo na walezi na watoto. Hii inajumuisha:

- kueleza kwamba tunachokijadili katika kipindi ni siri, na kwamba tutashirikisha taarifa hiyo kwa wengine kwa ridhaa ya mteja;
- kuainisha ni nani atakayejua matokeo ya kipimo cha VVU katika mazingira ya afya;
- elezea mazingira ambapo tutakiuka usiri, kwa mfano, iwapo sheria inasema kwamba ni lazima tutoe taarifa ya unyanyasaji wa kijinsia, au iwapo tutachukua hatua pale tunapoamini kwamba maisa ya yule mtoto au mtu mwingine yapo hatarini;
- kumsaidia mlezi na mtoto katika kuzichunguza faida na hasara za kushirikisha hali zao za maambukizo ya VVU kwa wengine;
- kuheshimu uamuzi wa watoto na walezi hao ambao hawataki kushirikisha hali zao za maambukizo kwa wengine;
- iwapo ni muafaka, kumsaidia mtoto na mlezi katika kushirikisha hali zao za maambukizo wanapojisikia kuwa tayari, kupanua wigo wao wa ushirikishaji shirikishi;
- iwapo kufanya kazi katika kikundi cha msaada, kuweka kanuni za kuwa na usiri shirikishi unaeleweka na kufuatwa na washiriki wote.

### Taratibu za kimaadili wakati wa kuwanasihi watoto na walezi wao

- Eleza kwamba wajibu wako ni kusikiliza, kuuliza maswali, na kumsaidia mtoto na mlezi kupata mantiki ya hali zao. Unaweza kutoa taarifa na unaweza kutoa mapendekezo, lakini hutamshauri au kumwambia ni kitu gani cha kufanya.
- Hakikisha kwamba kila kipindi ni sehemu ya usalama kwa ajili ya mtoto, ambacho ni mbali na kukatizwa-katizwa. Sema bayana ni wakati gani kipindi kitaisha, na fuata mipaka hiyo.
- Eleza na fuata usiri (kama hapo juu).
- Iwapo unahitaji kuukiuka usiri, kwanza mjulishe huyo mtoto na mlezi. Jadili nao na jaribu kuwajumuisha katika kufanya uamuzi.
- Wapatie rufaa watoto au walezi ambao wapo katika mtandao wako wa kijamii au wa kitaaluma (kwa mfano rafiki wa mtoto wako) kwa mnasihi tofauti.

- Ijue mipaka yako mwenyewe. Toa rufaa kwenda kwa mnasihi mwenzi au mtendaji wa ngazi ya juu kuliko wewe iwapo ujuzi zaidi unahitajika kwa faida ya mtoto.
- Dumisha umbali wa kitaaluma. Hii inajumuisha kutokufanya uhusiano wa kimwili usiyo muafaka na kusimamia mihemko yako ya kujihusisha ili iwe ndani ya uwezo wako, na isiingilie uwezo wako wa kuinasihi familia hiyo.
- Tumia vipindi na msimamizi au kiongozi wako ili kutafakari utendaji wako, na (wakati huohuo ukidumisha usiri) katika kujadili uchaguzi mgumu wa kimaadili na matatizo mengine yatokanayo na kazi yako.
- Hakikisha kwamba utambulisho wa mteja unalindwa iwapo suala lake linatumika kitaaluma kwa mfano katika utafiti au kuwasilishwa sehemu. Ni utendaji mzuri kubadilisha eneo la tukio kijiografia na pia majina.

## Kuwanasihi watoto kwa ajili ya kipimo cha VVU

Tunakisia kwamba unafanya kazi kama mnasihi kwa ajili ya kupima VVU, wewe ulikwisha kupima VVU. Unao utayari wa kujiweka ndani ya mchakato huo, na unajua namna ilivyokuwa kwako. Iwapo bado hujafanya kipimo cha VVU, tafadhali fanya hivyo kabla hujawanasihi wengine kuhusiana na kipimo hicho.

Sheria ya thamani kubwa kuhusiana na kipimo cha VVU ni kwamba ni hiari, siri na kinafanyika kwa ridhaa yako. Kuzitumia taratibu hizi ni tofauti kidogo kwa masuala ya watoto kuliko kwa watu wazima.

*Hiari.* Si mtu mzima ama mtoto analazimishwa kufanya kipimo hicho.

*Siri.* Taratibu za kawaida hutumika kuhusiana na kuweka majibu kuwa siri, lakini katika nchi nyingi majibu ya mtoto yanaweza kuwasilishwa kwa mlezi na mtoto kufichwa. Kwa maneno mengine, huwekwa kuwa siri kwa mtoto husika.  Ile sehemu moja ya mchakato wa unasihi kabla ya kupima huwa ni kwa ajili ya kumsaidia mlezi katika kuamua namna ya kusimamia ushirikishaji wa majibu ya mtoto huyo.

*Pakiwa na ridhaa.* Kwa kawaida inakuwa ni mlezi ndiye anahitajika kutoa ridhaa. Hii inamaanisha kuelewa hatari na faida, na ukweli kuchagua kufanya kipimo hicho, si tu kukubaliana na pendekezo la mfanyakazi wa afya. Mara tunapokuwa na ridhaa ya mlezi, ni lazima tutafute idhini (makubaliano) ya mtoto ili kuendelea na kufanya kipimo. Iwapo mtoto anakataa hapo kipimo hakiwezi kufanyika, kwani itakua si hiari.

Katika baadhi ya mazingira, pale ambapo mtoto mkubwa anahudhuria bila ya mlezi, inaruhusiwa kupata ridhaa kutoka kwa huyo mtoto. Kutegemeana na taratibu za sehemu tunamofanyia kazi, mazingira kama haya kuweza kujumuisha kama mazingira ya kubakwa, ujauzito na uwezekano wa hatari ya kupata VVU kwa bahati mbaya.

### Unasihi kabla ya kupima

Hapa chini tunaainisha hatua muhimu za kuchukua pale ambapo mlezi na mtoto wanakuja kwako kwa ajili ya unasihi wa kabla ya kupima. Tunapendekeza njia tofauti-tofauti za kushughulikia watoto wa umri tofauti, ila ni lazima uongozwe na uelewa wao na kupevuka kwao kama nyongeza kwenye umri wao. Tunatambua kwamba watoto wadogo na wale wachanga huo mchakato hufanyika wakiwa na mlezi, na panaweza kuhitajika kumhusisha mtoto kiasi au kutomhusisha kabisa.

Upimaji wa VVU kimsingi ni lazima ufanyike kwa faida ya mtoto. Kwa mfano, iwapo mtoto anaumwa na hapati nafuu, na tiba ya kupunguza makali ya VVU (ARV) inapatikana kwenye maeneo yetu kwa watu wanaoihitaji, hivyo kipimo hicho pengine kitakuwa cha manufaa kwa mtoto huyo, kugundua iwapo ni VVU au si VVU vinasababisha kuugua huko. Au, iwapo mtoto amegusana na VVU, na anataka kujua hali yao ya maambukizo, kwa hivyo kupima inakuwa ni pendekezo lake ili mradi ana msaada wa kutosha wa kuhimili hisia na kuhimili majibu na taathira zake. Japokuwa, zipo hatari, kwamba sisi au walezi tunaweza kutaka mtoto apimwe kwa sababu za hofu na shauku zetu wenyewe, badala ya kufikiria kwanza kuhusu mtoto huyo. Kwa hiyo tunahitaji kutafakari hisia zetu wenyewe, na kuwa makini kudadisi motisha wa kila mlezi kutaka mtoto apimwe.

Sababu za kwa nini unaweza usimpime mtoto baada ya unasihi wa awali zinajumuisha:

- mihemko mikali ya wasiwasi, kwa mfano mlezi au mtoto kushindwa kushiriki kikamilifu katika kipindi, na kuwa na uwezekano mkubwa wa kutohimili matokeo ya kuwa na ambukizo;
- hatari ya waziwazi kuhusu usalama wa mtoto huyo, kwa sababu mtoto au mlezi huyo ametamka wazi kwamba majibu ya kuwa na ambukizo yana uwezekano wa kuchochea mwitikio wa ukali kutoka kwa mwanafamilia;
- mtoto hana msaada wa kijamii kumsaidia kuhimili matokeo ya kuwa na ambukizo na taathira zake;
- mtoto kutokutoa idhini yake kwa ajili ya kipimo.

> Warsha za *Kivuko na Watoto* zinashughulikia masuala haya, kuwawezesha watoto na walezi kuelewa na kukubali VVU, na kujenga mazingira chanya zaidi kwa ajili ya walioathiriwa na VVU.

### *Unasihi wa kabla ya kupima kwa ajili ya walezi na mtoto*

| ***Kufanya kazi kwanza na mlezi pekee*** |
|---|
| Eleza kwamba kile mtakachojadili pamoja ni siri, na ni kwa namna gani na lini panaweza kuwepo utofauti na hali hii. |
| Jadilini ni kwa nini anapenda mtoto huyo apimwe VVU. Gundua iwapo mtoto amegusana na VVU. |
| Pata uelewa akilini mwako kiasi mlezi huyo anachojua kuhusu VVU na UKIMWI, na sahihisha yale yaliyo potofu. Ni nini wamekwisha kumwambia mtoto, na anataka mtoto ajue kiasi gani? |
| Jadilini na ueleze faida na changamoto za kujua hali ya ambukizo la VVU la mtoto. |
| Dadisi njia za kumjumuisha mtoto katika uamuzi wa kufanya kipimo, na katika kujua majibu. Tazama zile faida na hasara za kumjumuisha kiasi au kikamilifu, na jaribu kuainisha uwiano. Eleza kwamba, katika mazingira ya aina nyingi, watoto hufaidika kwa kuwa na taarifa, ilimradi iambatane na msaada. |
| Jadilini namna ambavyo jibu la kuwa na ambukizo la VVU litakavyo mwathiri mlezi na mtoto. Pia jadili namna ambavyo jibu la kutokuwa na ambukizo la VVU linaweza kuwaathiri (kwa mfano linaweza kumfanya mtoto kujisikia mkosefu iwapo mdogo wake ana VVU). |
| Iwapo inaonekana kwamba kupima kunaweza kumfaidisha mtoto, na mlezi wanataka kuendelea na kufanya kipimo hicho, mkaribishe mtoto aje kwenye kipindi.<br>Iwapo faida kwa ajili ya mtoto ni za mashaka, usiendelee; badala yake, pendekeza mkutano mwingine ndani ya kipindi cha miezi sita ili kufanya mapitio ya afya ya mtoto.<br>Iwapo mlezi hataki kuendelea, na mtoto inawezekana amegusana na VVU, wakaribishe waje kwenye kipindi kingine cha unasihi kabla ya kupima ndani ya kipindi cha miezi inayofuatia. |

<table>
<tr><th colspan="3">Kufanya kazi na mtoto na mlezi pamoja</th></tr>
<tr><th>Kwa watoto wa umri wa miaka 3 hadi 5</th><th>Kwa watoto wa umri wa miaka 6 hadi 12</th><th>Kwa watoto wa umri wa miaka 12</th></tr>
<tr><td colspan="3">Tabasamu na msaidie mtoto huyo ajisikie huru kwa kucheza na kupiga gumzo.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Eleza kwamba kile mnachojadili pamoja ni siri, na ile tofauti na hapo.</td></tr>
<tr><td>Ruhusu mlezi ajadili shauku zake na mtoto na mhamasishe mtoto atoe mwitikio.</td><td colspan="2">Mruhusu mlezi ajadili shauku zake na mtoto, na hamasisha majadiliano miongoni mwao.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Dadisi kujua mtoto anajua kitu gani kuhusu ni kwa nini wapo hapo. Sahihisha chochote kilicho potofu.</td><td>Dadisi kujua mtoto anajua kitu gani kuhusu ni kwa nini wapo hapo, na ni nini anakijua kuhusu VVU na UKIMWI. Sahihisha chochote kilicho potofu. Iwapo mtoto anaelekea kuzuiwa, pendekeza kwamba mlezi atoke nje ya kipindi.</td></tr>
<tr><td>Iwapo ni muhimu, eleza kwa kutumia lugha muafaka, kwa mfano;  ‘Je, ulijua kwamba vijidudu vinaweza kuingia katika damu ya watu? Kwa bahati, iwapo tunajua kwamba vijidudu vipo, na vinamfanya mtu kuugua, tunaweza kutumia dawa kuvidhibiti. Halafu mtu anaweza kuwa na afya njema. Kwa hiyo ni vema kufahamu iwapo vijidudu vipo au hapana. Kama tukichukua damu kiasi kidogo kutoka kwako wewe tunaweza kugundua kama una vijidudu vya aina fulani.’</td><td>Iwapo ni muhimu, eleza kwa kutumia lugha muafaka, ukizungumza kuhusu ‘kijidudu’, kirusi’, au VVU, kuendana na kile kiasi huyo mtoto anachojua na kile mlichokubaliana na mlezi. Eleza faida na changamoto za kujua iwapo kuna kitu fulani katika damu yetu.</td><td>Iwapo ni muhimu, eleza kuhusu VVU na upimaji wa VVU na faida na changamoto za kujua hali yako mwenyewe ya ambukizo la VVU.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Eleza namna ambavyo damu huchukuliwa, inachukua muda gani kufanya kipimo hicho, na majibu yawezekanayo yanamaanisha nini.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Jadili namna ambavyo majibu yatashirikishwa, ni nani atatoa msaada kwa mtoto huyo iwapo ana VVU na, iwapo kwa hali hii, ni kwa namna gani atapata matunzo na tiba wakati itakapohitajika.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Uliza iwapo mtoto ana maswali yoyote au shauku, ikijumuisha kuhusu faida za kufanya kipimo cha VVU. Toa majibu ya kweli ambayo anaweza kuyaelewa.</td></tr>
<tr><td>Mwulize mtoto ‘je tutafute kujua iwapa vijidudu vimo katika damu yako?’</td><td>Mwulize mtoto ‘je tutafute kujua kama kuna kitu chochote katika damu yako?’</td><td>Mwulize mtoto ‘je tutafute kujua iwapo VVU vipo katika damu yako?’</td></tr>
<tr><td colspan="3">Iwapo mtoto anaridhia (anakubali), tafuta riddaa kutoka kwa mlezi. Sisitiza kwamba ni muhimu kurudi tena kwa ajili ya majibu.<br>Iwapo mtoto anakataa, wakaribishe kwa ajili ya kipindi kingine tena.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Iwapo ni muafaka, eleza kuhusu huduma nyingine, au mpe mteja rufaa kwenda huko kwa ajili ya huduma hizo, kwa mfano huduma za afya ya uzazi.</td></tr>
</table>

### *Unasihi wa kabla ya kupima kwa watoto wanaohudhuria peke yao*

Kwenye mazingira ambapo mtoto anahudhuria unasihi wa kabla ya kupima akiwa peke yake, utahitaji kuhakiki iwapo ana uwezo wa kutoa ridhaa katika kufanya kipimo cha VVU, kwa kulingana na sheria za eneo na kupevuka kwao kihisia. Ili kutoa ridhaa, mtoto huyo ni lazima:

- aelewe hatari na faida za upimaji zinazowezekana kuwapo;
- awe na utayari wa kukubali msaada katika kukabiliana na majibu ya kipimo, hasa iwapo kitaonesha kuwa na ambukizo.

Iwapo kisheria na kihisia anao uwezo wa kutoa ridhaa, utafuata hatua zilezile za kufanya kazi na mlezi. Uliza iwapo ana weza kufikiria mtu ambaye atampa msaada iwapo majibu ni kwamba ana ambukizo, na nani ataandamana naye katika unasihi wa baada ya kupima.

Iwapo mtoto huyo kisheria hawezi kutoa ridhaa, fuata hatua zilezile, lakini eleza kwamba kuweza kupata huduma ya kupima, iwapo bado anataka, atahitaji kurudi akiwa na mlezi. Iwapo mtoto anasita kuja na mlezi wake wa msingi, dadisi ni kwa nini. Pengine unaweza kusaidia kwa kuwa na mkutano na mlezi na kumsaidia. Mbadala wa hivyo, dadisi iwapo mtoto huyo anaye mtu mwingine katika mtandao wao wa msaada ambaye anaweza kuchukua jukumu la mlezi. Iwapo ndivyo, wakati unakutana na mtu huyo ni lazima ueleze ni kwa nini ameombwa achukue jukumu hilo, na ni lazima aafiki kuzingatia usiri.

Iwapo unahisi kwamba mtoto hawezi kutoa ridhaa kutokana na kukosa uelewa ama kutoridhia kupata msaada, mwambie arudi tena kwa ajili ya kipindi kingine ambapo mnaweza kuongelea zaidi jambo hilo.

### Unasihi wa baada ya kupima

Unasihi wa baada ya kupima huwasaidia walezi na watoto kuelewa majibu ya kipimo na vidokezo vyake, na kutafakari na kupanga ni nini kitokee baada ya hapo.

Namna ambavyo unaendesha kipindi cha unasihi baada ya kupima kutategemea na kile mlichokubaliana na mlezi na mtoto katika kipindi cha unasihi kabla ya kupima na fikra zao katika kipindi cha unasihi baada ya kupima. Kwa mfano, mnaweza kuwa mlikubaliana kwamba mtoto apate majibu kutoka kwako bila ya kuwapo kwa mlezi wake, kwamba wote wawili wasikie majibu kwa wakati huohuo kutoka kwako, au kwamba mlezi ashirikishe majibu kule nyumbani, wakati muda ukiwa sahihi.

Hapa ni maudhui ya jumla kwa ajili yako kutohoa. Hii ni kwaajili ya hali ambamo wewe unamwambia mlezi kwanza, na kisha unamleta mtoto katika kipindi ili ayasikie majibu hayo.

<table>
<tr><th colspan="2">Kufanya kazi na mlezi akiwa peke yake</th></tr>
<tr><td colspan="2">Hakiki iwapo anajua ni kwa nini amekuja, na kwamba yupo tayari kupokea majibu.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Toa majibu na eleza yanamaanisha nini. Kuwa na uhakika kwamba anaelewa.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Tao mwanya kwa ajili ya kutafakari, kujichunguza namna anavyojisikia kuhusu majibu hayo.</td></tr>
<tr><td>Kwa ajili ya majibu ya kutokuwa na ambukizo</td><td>Kwa ajili ya majibu ya kuwa na ambukizo</td></tr>
<tr><td>Hakiki iwapo anaelewa namna ambavyo VVU huambukizwa, na jadili namna ya kupunguza uwezekano wa mtoto kutopata ambukizo la VVU.</td><td>Jadili hatua za baada ya hapo kuhusiana na rufaa na unasihi. Sisitiza upatikanaji wa matunzo na msaada, na – lini vinahitajika– tiba yenye ufanisi ili kumsaidia huyo mtoto kuishi vyema na kuwa na watoto wake mwenyewe wasio na VVU.</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| Iwapo ni muafaka*, eleza kuhusu kipindi cha mficho na mahitaji ya kipimo kingine. | Fanya mapitio ya njia za kubakia wenye afya na kukwepa ambukizo hapo baadaye, na shughulikia hofu zozote ambazo mlezi anazo. |
| Jadili namna ya kushirikisha majibu kwa mtoto, ni nani atalifanya jambo hili, na ni lini. | |
| | Jadili kuhusu kushirikisha majibu kwa wengine; sisitiza kwamba hakuna haraka, mnaweza kuongea zaidi kuhusu mambo haya katika vipindi vinavyofuatia. |
| ***Kufanya kazi na mtoto na mlezi kwa pamoja*** | |
| Iwapo ni muafaka, mkaribishe mtoto kwenye kipindi. Tafuta kujua namna anavyojisikia, na hakiki iwapo yupo tayari kupokea majibu hayo. | |
| Toa majibu kwa kutumia masharti uliyoyatumia wakati wa unasihi wa kabla ya kupima, au mwache mlezi atoe majibu hayo. | |
| Hakiki iwapo mtoto ameyaelewa majibu hayo na mpatie muda wa kuuliza maswali na kuibua shauku zake. | |
| Iwapo ni muafaka*, eleza kuhusu kipindi cha mficho na mahitaji ya kipimo kingine. | Sisitiza kwamba pakiwa na tiba, matunzo na msaada, watu wanaweza kuishi muda mrefu na wenye afya njema na VVU: 'tutafanya kazi pamoja ili tuweze kuhimili jambo hili na kuishi vizuri.' Wahakikishie tena kwamba watoto wenye VVU wanaweza kukua hadi kuwa na watoto wao wenyewe ambao hawana VVU. |
| Jadili na mtoto huyo mambo anayoweza kufanya ili kuondoa VVU kutoka katika damu yake. | Jadili namna anavyojisikia huhusu kushirikisha. Eleza kwamba kuwaambia wengine kunaweza kuwa kwa manufaa, lakini kunaweza pia kusababisha matatizo pale ambapo wengine hawajui vya kutosha kuhusu VVU. Hakuna haraka, ni kitu cha kuongelea zaidi katika vipindi vya hapo baadaye. |
| | Wahakikishie tena kwamba hawako peke yao –wapo watoto wengine waliopo katika hali kama ya kwao. Panga rufaa katika kundi-rika la msaada, iwapo wengependa, na ufuatiliaji, na hakiki kwamba mlezi na mtoto wanazielewa hatua zinazofuatia hapo. |

Iwapo kipindi chako ni pamoja na mtoto mkubwa kidogo (ambaye alitoa ridhaa) na mlezi akiwa hayupo, hapo utafuata nusu ya kwanza ya hatua hizo hapo juu. Hakikisha unawapatia muda wa kujieleza, na kujadili hofu zao. Iwapo mtoto hajisikii kuwa tayari kupokea majibu, au hana msaada au utulivu wa kihisia ili kuhimili majibu, weka mpango wa kumwezesha kuwa tayari, na arudi kwa ajili ya kipindi kingine.

Katika hali ya majibu yasiyoonesha dhahiri (hayaeleweki), fuata mchakato ule ule lakini eleza kwamba majibu hayakueleweka, na kwamba kipimo kinahitaji kurudiwa tena ndani ya muda wa wiki mbili. Sisitiza kwamba bado hatujui hali ya ambukizo la mtoto huyo. Majibu hayo ambayo si dhahiri yanaweza kuwa ni kwa sababu ya matatizo katika maabara, au kwa sababu mtoto bado yupo katika hatua

*** Iwapo mtoto ana majibu ya kutokuwa na ambukizo, ni wakati gani utampima tena?**

Ushauri wa Shirika la Afya Duniani (WHO) ni kuwapima tena watu ambao: ni wajawazito; wana hatari ya udumishwaji wa kugusana na VVU (ikijumuisha kunyonyeshwa kutoka kwa mtu mwingine ambaye ana VVU); wamepitia ajali maalumu ya kujihatarisha na VVU katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Watoto pia wanaweza kurudia kupima kutokana na wasiwasi. Iwapo kuwahakikishia na kuchunguza hofu zao hakufanyi kazi, kuwapima tena kunaweza kupunguza wasiwasi wao.

ya awali ya kuwa na VVU, wakati ambapo ni rahisi kusambaza VVU kwa mtu mwingine. Kwa hiyo ni muhimu kukwepa uwezekano wa kuambukiza. Huu muda wa nyongeza kwa uhakika utakuwa wenye mfadhaiko kwa mteja wako, kwa hiyo mpatie muda aongee kuhusu shauku zake, na hamasisha arudi kwa ajili ya kupima tena.

## Ushirikishaji wa hali ya maambukizo ya VVU wakati fulani baada ya kupima

Ni jambo la kawaida kwa walezi kufanya watoto wapimwe VVU, kujua kwamba mtoto ana VVU, lakini si kuhamisha taarifa hiyo kuifikisha kwa mtoto husika. Vivyo hivyo, walezi wanaweza wasishirikishe hali zao wenyewe za kuwa na ambukizo la VVU kwa watoto wao. Zipo sababu lukuki za kubakia kimya. Kwa jumla, japokuwa, ni vizuri zaidi kwa mtoto kujua hali za ambukizo la VVU lao wenyewe na la mlezi wao, haswa kadiri wanavyozidi kukua, ilimradi wanapata msaada kwenye kuelewa na kuhimili hali hiyo na kuishi kwa matumaini.

**Kisanduku 1 Kisa Mkasa: Kumshirikisha mtoto wakati fulani baada ya kipimo cha VVU**

Katika warsha moja ya *Kivuko na Watoto* mtoto wa umri wa miaka 10 mwenye VVU, ambaye hakujua hali yake ya maambukizo, alisema 'Iwapo ningekuwa na VVU ningependa kujiua.' Kipindi cha VVU kilikuwa siku chache tu baadaye. Watoto wote na walezi walijifunza tofauti kati ya VVU na UKIMWI, na namna ambavyo tiba inaweza kuwasaidia watu wanaohitaji kubakia wenye afya na kuishi maisha ya furaha na uzalishaji. Siku chache baada ya hapo, mlezi wa mvulana yule alimwambia kwamba alikuwa na VVU. Mwitikio wake wa papo kwa papo ulikuwa kwamba 'Je mimi nina VVU au nina UKIMWI?'. Alimjibu kuwa 'wewe una VVU kwa sababu unatumia tiba yako kwa usahihi sana na hiyo inavifanya VVU visikufanye uugue. Kwa hivyo unaendelea vizuri mno.' Yule mvulana alijibu 'Hiyo ni SAWA basi', na akaondoka kwa furaha kwenda kucheza mpira wa miguu na rafiki zake. Yule mlezi alifurahishwa na kupungukiwa na mzigo kutokana na kushirikishana siri na yule mvulana.

Yapo mazingira ya aina nyingi ambamo unaweza kuchukua jukumu muhimu sana, kuwezesha patokee ushirikishaji kwa mtoto kuhusu hali ya ambukizo la VVU la mlezi au mtoto mwenyewe.

- Mlezi anaweza kukufuata kwa ajili ya msaada, akifikiri kwamba anataka kumwambia mtoto au kwamba mtoto anataka kujua, lakini akiwa hana uhakika kuhusu namna ya kufanya hivyo.
- Mtoto anaweza, wakati anahudhuria kliniki kwa ajili ya vipimo na tiba, akauliza ni kwa nini wanalazimika kutumia dawa. Yule mfanyakazi wa afya hataweza kumwambia mtoto moja kwa moja – hii itakuwa ghafla mno, na ingekuwa bila ushirikiano wa mlezi – lakini kama sehemu ya kazi yake ya matunzo kwa mtoto ni lazima awezeshe mtoto huyo apate jibu. Katika hali hii huyo mfanyakazi wa afya atamtaka mlezi wakutane na mnasihi ili kujadili ushirikishaji.
- Mfanyakazi wa afya anaweza kutaka mtoto ajue hali yake mwenyewe ya ambukizo kwa sababu pana uwezekano wa kumsaidia. Ushirikishaji unaweza kusaidia kwa njia nyingi: hiyo taarifa itapunguza msongo na wasiwasi kwa watoto ambao wanahisia fulani kuhusu hali zao za ambukizo, au zile za walezi wao; inamwezesha mtoto kupata msaada kutoka kwa wenzake; na kuwa na taarifa kamili kunaweza kuwasaidia hao ambao wapo kwenye tiba kuwa na ufuasi mzuri zaidi. Lakini, ni mwiko mfanyakazi wa afya au mnasihi kulazimisha mtazamo wao kwa wale waliopo chini ya uangalizi wao.

Ni lazima tuwe tunatambua zile hasara zinazowezekana kuwapo katika ushirikishaji kwa watoto. Hizi zinajumuisha mtoto huyo kupata usununi, na kuwa na hasira na kuchukia kuja kwako, yote haya kwa kuhusiana na hali yake ya ambukizo na pia ukweli kwamba hii imekuwa ikifichwa

kwake. Ipo pia hatari kwamba mtoto atakabiliana na unyanyapaa na ubaguzi kutokana na kuwashirikisha wengine.

Kipindi 13 ni kuhusu upimaji wa VVU na kuongelea kuhusu VVU na watoto. Kinajumuisha baadhi ya rasilimali nzuri kwa ajili ya wanasihi, ikijumuisha hofu na faida zinazohusiana na kushirikisha watoto kuhusu ugunduzi wa VVU, na msaada kwa walezi kuhusu namna ya kuwataarifu watoto wao.

Uwe na uhakika wa kujua taratibu nchini mwako na sera za kwenye shirika lako kuhusiana na ushirikishaji kwa watoto. Kwa mfano, katika baadhi ya nchi wafanyakazi wa afya wanaruhusiwa kuongea na watoto kuhusu hali ya ambukizo bila ridhaa ya walezi wao, isipokuwa kwa watoto ambao tayari wamepevuka kingono, wajawazito au walioolewa. Lakini, taratibu hizi huenda kinyume na haki za watoto za kupatiwa taarifa kuhusu afya zao wenyewe. Kama wanasihi, wajibu wetu ni kufanya kazi na walezi ili kugundua suluhu nzuri kuliko zote kwa ajili ya hali zao. Hapa ni badhi ya hatua za kufuata.

<table>
<tr><td colspan="3">Weka bayana kile ambacho mlezi amekwisha kumwambia mtoto kuhusiana na afya yake na hali ya ambukizo la VVU.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Dadisi mawazo na hisia za huyo mlezi kuhusiana na hali hiyo.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Dadisi kuhusiana na faida na hasara ziwezekanazo za kushirikisha kwa mtoto huyo (angalia Zoezi 13.6).</td></tr>
<tr><td colspan="3">Dadisi kuhusu faida ziwezekanazo za kutokumshirikisha mtoto huyo (kwa mfano kwamba mtoto huyo angekuwa kapunguza wasiwasi) na hasara ziwezekanazo (kwa mfano anaweza kugundua kutoka kwa mtu mwingine kwa bahati mbaya). Hii inaweza kuchukua vipindi vingi; mlezi ni lazima ajisikie mwenye hali ya kuwa na madaraka ya kumudu, na bila kukandamizwa.</td></tr>
<tr><td>Mlezi anaamua kutoshirikisha</td><td>Mlezi hawezi kuamua</td><td>Mlezi anaamua kushirikisha</td></tr>
<tr><td>Heshimu maamuzi yake.</td><td>Mkaribishe aje kwa ajili ya kipindi kingine.</td><td>Mpatie msaada katika kupanga namna ya kufanya hivyo (angalia Zoezi 13.7). Hii inaweza kujumuisha kufanyia mazoezi kupitia igizo.</td></tr>
<tr><td>Mhamasishe afikiri kuhusu jambo hili kwa mara nyingine tena hapo baadaye, kadiri mtoto anavyokua na hali kubadilika.</td><td>Muunganishe na kikundi cha msaada ambamo anaweza kukutana na walezi wengine na kugundua uzoefu wao.</td><td>Karibisha mlezi na mtoto warudi tena kwa ajili ya vipindi vya mwendelezo.</td></tr>
</table>

## Unasihi wa msaada kwa watoto wenye VVU na walezi wao

Madhumuni ya uhakika ya unasihi wa mwendelezo ni kutoa msaada kwa mtoto anayeishi na VVU kuhimili na kuishi vyema.

Katika kutoa mwitikio kwa hali yake ya ambukizo la VVU, watoto na walezi wanao uwezekano wa kupitia katika hatua tano zinazotambulika za kukabiliana na kuomboleza na kupoteza. Hizi zinajumuisha kukataa, kujadili namna ya kukubaliana, hasira, kukata tamaa, na kukubaliana. Kumbuka, wanaweza wasipitie katika katua zote hizi kwa mpangilio huu, na wanaweza kurudia hatua fulani. Hii ni kawaida na hakuna mpangilio maalumu. Kama mnasihi madhumuni yako ni kumsaidia mtoto na mlezi katika kufikia ile hatua ya kukubaliana, ili waweze kuishi vizuri na VVU.

### Mara baada ya kushirikisha

Hapa ni pale ambapo ushiriki wako utakuwa mkubwa zaidi. Kwa ukamilifu kabisa utapanga na mtoto na mlezi tarehe kwa ajili ya vipindi vya ufuatiliaji, hasa iwapo mwitikio wao unaashiria wanahitaji au kutaka msaada.

Katika hatua hii ni muhimu sana kushughulikia na kutatua masuala yawezekanayo kuwapo ya hasira na lawama, ambayo yanaweza kuhisiwa na wote wawili mlezi na mtoto. Jaribu kuhakikisha kwamba mtoto ana mtu fulani anayeweza kuongea naye zaidi ya wewe, kwa mfano mlezi, ndugu mwingine, au rafiki, ambaye unaweza kumwainisha kabla ya ushirikishaji. Unaweza kuwaambia kuhusu vikundi vya msaada ambavyo wanaweza kuhudhuria.

### Unasihi endelevu

Kupitia unasihi endelevu wako kwa ajili ya huyo mtoto na, iwapo ni muafaka, mlezi, unadhamiria:

- kuwasaidia wakubali ukweli wa kuishi na VVU;
- kugundua na kukabiliana na hofu na shauku zao;
- kuhakikisha kuwa wameelewa kwamba *hakuna mwenye hatia* kutokana na wao kuwa na VVU;
- kuwasaidia katika kufikiria iwapo wanataka kushirikisha hali zao za maambukizo kwa wengine na, iwapo ndivyo, kwa nani, na kwa namna gani watafanya hivyo;
- kuwaambia kuhusu uchaguzi wa misaada kutoka kwa makundi ya wenzao, iwapo yanapatikana maeneo yao;
- kuwapatia taarifa muafaka kuhusu VVU na masuala mengine kama yanavyojitokeza, kama vile afya ya uzazi;
- kumuunganisha mtoto kwenye huduma za msaada zinazopatikana –kitabibu, kisaikolojia na za kiroho – ili kupanua rasilimali zao za msaada;
- kumsaidia mtoto katika kuelewa tiba –wakati wanaihitaji, namna inavyosaidia afya zao, na ni kwa nini ni muhimu kutumia dawa kila mara – ili waweze kuishi vyema na VVU;
- kumsaidia mtoto kujenga ari zake  za ndani, mtazamo chanya katika maisha, na matarajio na mipango yao ya hapo baadaye.

> Zoezi 14.3 linawasaidia walezi na watoto kukabiliana na hofu zao kuhusiana na kuambukiza au kupata VVU.

Wakati unatoa unasihi wa usaidizi ni lazima:

- ufanye kazi na mtazamo chanya na kuonesha kufanikisha na kuwahakikishia tena hivyo;
- kutambua kwamba mtoto anapitia hali yenye kiwewe;
- jaribu kuhakikisha kwamba mtoto huyo anapata matunzo yenye mjumuisho wa vitu vyote;
- andaa mazingira salama na yenye usiri;
- iwapo inawezekana, fanya kazi na mlezi ambaye atatenda kama msingi wa ulinzi kwa ajili ya huyo mtoto;
- tafuta msaada pale mahitaji yanapojitokeza.

## Kuwanasihi watoto katika masuala maalum

### Usiri na kushirikisha

Kama sehemu ya utendaji wa kawaida, tunahakikisha kwamba tunawafanya wateja wetu waelewe zile taratibu sisi na watendaji wenzetu tunazozitumia kuhusiana na usiri.  Pia tunaandaa

mazingira ambamo tunakiuka usiri. Nyongeza ya hapo, tunahitaji kuwasaidia watoto katika kufikiria namna ambavyo watasimamia hiyo taarifa ya hali yao wenyewe ya VVU. Hapa ni baadhi ya mambo muhimu ambayo watoto wanahitaji kufikiria, pamoja na uwezeshaji wako.

- Inaweza kutusaidia kuishi vyema na VVU iwapo tunaweza kufikiria kuhusu mtu mzima anayeaminika au rafiki wa karibu ambaye tunaweza kumwita na kumwambia. Hapo tunaye mtu fulani wa kuongea naye kuhusu VVU pale ambapo tunahisi kuwa na wasiwasi. Kumwambia mtu fulani kuwa tuna VVU hujulikana kama 'kushirikisha'.
- Hatua za kwanza kuelekea katika kushirikisha ni kwamba tunahitaji kujua ukweli kuhusu VVU, na kuelewa VVU ni kitu gani na ni kitu gani ambacho si VVU.
- Mara nyingine tunaweza kuamua kutokuwaambia wengine. Hii si kwa sababu kuna chochote kibaya kuhusu kuwa na VVU; hatuhifadhi taarifa hii sisi wenyewe kwa sababu tunaona aibu. Ni kwa sababu watu wengine wanaweza bado wasiwe na taarifa iliyo sahihi au uelewa kuhusu VVU na UKIMWI. Iwapo hawaelewi vizuri wanaweza kutenda vibaya, katika njia ambazo zinaweza kutuumiza.
- Mara uwaambiapo watu wengine, huwezi kurudi nyuma na kutowaambia. Pia, huwezi kujua itakuwa na athari gani. Zinaweza kuwa chanya ama hasi, au yote mawili.
- Unaweza usihitaji kuweka siri kwa asilimia 100. Kuna uwezekano wa kutengeneza 'siri shirikishi'; hii ikimaanisha kushirikisha hali yako ya ambukizo kwa watu unaowaamini, ambao hawatamwambia mtu mwingine yeyote bila ruhusa yako. Warsha za *Kivuko na Watoto* huunda jamii ya watu wanaoelewa kuhusu kuishi na VVU na ambao husaidiana.
- Watu wengi hugundua kwamba kujiunga na kundi rika la msaada la watu wazima au watoto ni jambo la msaada, kwani unaweza kuongea na watu wanaopitia masuala yanayofanana.

**Unasihi kwa ajili ya tiba ya dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs)**

Ni muhimu kuwaeleza walezi kwamba njia ya kwanza ya kumtibu mtu yeyote mwenye VVU, ikijumuisha watoto, ni kuwapa upendo, matunzo na msaada, chakula chenye virutubisho, makazi salama, pale inapowezekana, mazoezi. Hizi ndizo nguzo za misngi za tofali katika ujenzi wa afya nzuri. Dawa hufanya kazi kwa ufanisi wakati misingi hii imekaa vizuri mahali pake.

Kuwasaidia watoto na walezi katika kuzifikia na ufuasi wa dawa, wakati miili yao inazihitaji, ni sehemu muhimu katika unasihi wa kuendelea. Utahitaji:

- kushirikishana taarifa na wateja kuhusu ni wapi pa kupata dawa za kupunguza makali ya VVU (dawa za Anti-Retroviral, au ARVs), namna gani dawa hizi zinafanya kazi, na umuhimu wa kufuatilia ufanisi wake katika miili yetu;
- kuwasaidia wafanye ARVs kuwa ni sehemu ya mpangilio wa kila siku kwa kuunganisha kile kitendo cha kuzimeza kila siku na jukumu la kila siku la kupiga mswaki, kuvaa nguo, au kula chakula cha usiku;
- kutumia njia rahisi zisizotishia za kueleza namna ambavyo VVU huathiri miili yetu na mfumo wa kinga na namna ambavyo ARVs huwasaidia watu wenye VVU kubakia wenye afya, kwa mfano; 'mfumo wa kinga upo kama kikundi cha wakulima wanao ondoa magugu ili mazao yashamiri vizuri. VVU hujaribu kuwazuia wakulima hao kuondoa magugu, lakini tiba huwawezesha kuendelea';
- kuwahamasisha na kuwapa msaada watoto katika kutumia ARVs mara kwa mara: eleza kwamba kutomeza ARVs mara kwa mara husababisha kuugua, na kwamba VVU katika miili yetu vinaweza kujenga usugu wa dawa;

> Soma Zoezi 14.7 ili kujifunza zaidi kutoka kwa watoto wanaoishi na VVU kuhusu nini kiliwasaidia katika kutumia dawa zao mara kwa mara.

- kuchunguza kujua iwapo wateja wanameza ARVs mara kwa mara kwa kutumia mrejesho wao, kuzihesabu dawa, na viashiria vya kitabibu kama vile wingi wa  CD4 zao na wingi wa virusi;
- kudodosa watoto na walezi matatizo yoyote wanayoweza kuwa nayo kuhusiana na kumeza ARVs mara kwa mara, ikijumuisha sumu na athari zitokanazo na tiba, na awasaidie kuweka mikakati ya kukabiliana na matatizo kama haya;
- kuwapatia rufaa kwenda kwa mamlaka husika katika masuala yanayojitokeza kwenye maeneo ya huduma za afya (kwa mfano; wafanyakazi wasio rafiki, kuomba wa rushwa).

### Kuwanasihi watoto walionyanyaswa

Kwa jumla, watoto walionyanyaswa wana uwezekano wa kuwa na tabia tofauti na watoto ambao hawajanyanyaswa. Unaweza kutambua, kwa mfano, mtoto ambaye kwa uhakika anajitenga, ambaye hagusani macho na mtu, na ambaye anashindwa kuongea kuhusu hisia zake. Hapa ni aina kuu za unyanyasaji wa mtoto na ishara za kutafuta.

| Aina ya unyanyasaji | Ishara za unyanyasaji |
|---|---|
| **Kutojali** ni kushindwa kutoa chakula, mavazi, malazi, matunzo ya kitabibu na usimamizi kwa kiwango ambacho kaya inaweza kumudu kufanya. | • mtoto ni mchafu, ana mavazi yasiyostahiki<br>• kadumaa kwenye kukua<br>• kuwepo kwa matatizo ya kiafya yanayotibika<br>• hayupo shule |
| **Unyanyasaji wa kimwili** huhusisha ushari wa maneno na vitendo vinavyoelekezwa kwa mtoto.<br><br>Jedwali 9.1 linaonesha tofauti kati ya kuwaadhibu watoto (mf. kuwapiga) na kutumia nidhamu chanya; hii inaweza kukusaidia wewe unapowanasihi walezi ambao hutumia adhabu ya kimwili. | • mikato, majeraha ya moto, michubuko na majeraha ya kuteguka<br>• mtoto amedhuriwa kwa zaidi ya ‘ajali,’ zaidi ya ilivyo kawaida<br>• hofu ya mtu wa aina fulani au kitu fulani |
| **Unyanyasaji wa kihisia** hujumuisha kukosolewa kunakozidi kiwango, kuitwa majina, kudharauliwa, uharibifu wa vitu binafsi, kudhalilishwa, na kusitisha mawasiliano na upendo. | • wasiwasi<br>• ari iliyoshuka<br>• usununi<br>• kujitenga kando (kuwa mbali na ukweli)<br>• matumizi ya dawa za kulevya na/au pombe<br>• hasira<br>• kujiumiza (kwa mfano; kujikata mikononi)<br>• ngono za umri mdogo na ngono za ovyo-ovyo |

| Aina ya unyanyasaji | Ishara za unyanyasaji |
|---|---|
| **Unyanyasaji wa kimapenzi** unajumuisha kuonesha isivyo sahihi via vya uzazi, kuwaonesha watoto picha za utupu, kutengeneza picha za utupu na mtoto, mguso wa kingono, kufanya ngono, na kuuza watoto kwenye huduma za ngono.<br><br>Zoezi 26.3 lina linganisha kujali na miguso ya kimapenzi, ambalo linaweza kukusaidia wewe kugundua na kupima kama mtoto ananyanyaswa. | • Kupandwa sana na hasira, wepesi wa kupandwa na hasira na kulia<br>• hofu ya mtu fulani au kitu fulani<br>• tabia isiyo na heshima<br>• kuweweseka na kukojoa kitandani au kuchafua<br>• kujizoesha kwa wingi sana katika masuala ya ujinsia kuliko inavyotarajiwa katika umri wake<br>• maumivu kwenye uke au sehemu ya haja kubwa, kutokwa na damu au kuwashwa<br>• kutembea au kuketi kwa shida<br>• ujauzito |

Tambua kwamba kuwapo kwa ishara hizi haikuhakikishii kwamba mtoto ananyanyaswa; mtoto mwenye wasiwasi au anayejitenga anaweza kuwa ni mwenye aibu kiurahisi tu na kuathiriwa na matatizo yaliyopo katika maisha yake, kama vile kupotelewa na mzazi(wazazi). Lakini, kuwapo kwa dalili hizi humaanisha kwamba ni lazima uangalie kwa makini zaidi.

Iwapo unatilia mashaka kwamba mtoto huyu ananyanyaswa ungeweza:

- kuchunguza suala hilo ukiwa na mtoto wakati ambapo mlezi hayupo:
    - o uliza maswali ya kistaarabu, au chunguza kwa kutumia hadithi au mchezo, lakini usibishane na huyo mtoto au kujaribu kumlazimisha kuongea kuhusu jambo hilo;
    - o peleka wazo kwamba pale ambapo mtoto anafanyiwa ukatili (kama vile mtoto aliye kwenye hadithi unayoisimulia) si kosa lake hata kidogo; ni wajibu wa watu wazima kuwalinda watoto;
    - o eleza kwamba pale ambapo watu wazima wanashindwa kumlinda mtoto kitu fulani kinahitajika kibadilike; wahakikishie tena (kwa mfano kupitia hadithi yako hiyo) kwamba hatua zinaweza kuchukuliwa, unyanyasaji unaweza kukoma, na afya ya mtoto inaweza kuboreshwa;
- chunguza wasiwasi wako ukiwa na mlezi wakati ambapo mtoto hayupo;
- chunguza jambo hilohilo ukiwa na wote wawili; mtoto na mlezi iwapo mlezi si yule mtu anayefanya unyanyasaji huo.

> Zoezi 26.4 linajumuisha mawazo kuhusu vitu ambavyo watoto wanaweza kufanya ili kujilinda wao wenyewe dhidi ya unyanyasaji wa kimapenzi, na vitu ambavyo walezi wanaweza kufanya kuzuia unyanyasaji huo.
>
> Unaweza kutumia Zoezi 26.5 kumsaidia mtoto afanyie mazoezi njia mbalimbali ambazo wangeweza kuzitumia kutoa miitikio katika kufuatiliwa kwa nia ya kuwadhalilisha.

Iwapo mtoto anakuambia kwamba anafanyiwa unyanyasaji ni lazmia umwamini; ni mara chache sana watoto hudanganya kuhusu kufanyiwa udhalilishaji, hasa unyanyasaji wa kimapenzi (weka akilini kwamba wanyanyasaji mara nyingi huwaambia watoto kwamba hakuna haja ya kumwambia mtu yeyote kwani hakuna atakayewaamini). Ni lazima usioneshe mshtuko, ila toa mwitikio ulio na ujumbe huu ufuatao:

1. Ninakuamini.

2. Ninafurahia ulichoniambia.

3. Pole jambo ilo limekutokea.

4. Si kosa lako jambo hili kutokea kwako.

5. Ninahitaji kujua zaidi ili kujua njia bora ya kukusaidia.

Ongea na mtoto kuhusu nani mwingine atahitaji kuambiwa (kwa mfano iwapo wewe kisheria unawajibika kutoa taarifa ya unyanyasaji huo) na nani mwingine anadhani anahitaji kujua. Eleza wazi kwamba nini kinatakiwa kutokea baada ya hapa, kutokana na matokeo ya unyanyasaji huo, na ni ulinzi wa namna gani na msaada unapatikana.

Iwapo mtoto anao utayari wa wewe kujadili suala hili na mlezi, wakaribishe katika kipindi na wezesha majadiliano miongoni mwa mtoto na mlezi kuhusu nini kifanyike baada ya hapa.

- Iwapo polisi wanahusika unaweza kuhitaji kumpa mtoto rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu (pakiwepo na ridhaa ya mlezi) kwa ajili ya ushahidi wa unyanyasaji wa kimwili au kimapenzi.
- Iwapo ni muafaka, na ukiwa na ridhaa ya mlezi, fanya mpango wa kinga ya ambukizo la VVU (ijulikanayo pia kama PEP, ili kupunguza uwezekano wa kupata VVU) na uzuiaji mimba wa dharura kwa ajili ya mtoto, na pia upimaji na kutibu magonjwa yaambukizwayo kwa ngono, ikijumuisha VVU.

Iwapo mlezi au mwenzi wake ndio mhalifu wa unyanyasaji huo utahitaji kumsaidia mtoto katika kufikiria ni kitu gani cha kufanya. Unaweza kuhitaji kutoa taarifa kuhusu unyanyasaji huo. Ikiwezekana, mlete mtu mzima mwingine wa tofauti kwenye majadiliano, ambaye mtoto anamwamini. Madhumuni yako ni kumsaidia mtoto katika kufikia hali ambayo unyanyasaji huo hautokei tena, au anaweza kuukwepa, au kuupunguza. Jitahadharishe kwamba unyanyasaji huu unaweza kuongezeka iwapo mhalifu anayesemwa na mtoto kutopewa ulinzi dhidi yake.

## Kumnasihi mtoto kuhusiana na kifo na kufariki

Mara nyingine mnasihi ni lazima awasaidie watoto katika kuhimili kifo au kusogezwa karibu na kifo cha mzazi, mdogo wake au rafiki, au kifo chake yeye mwenyewe. Tunahitaji kuwasaidia waelewe kifo kama ukweli katika maisha, na kuwapa msaada katika zile hatua za kukabiliana na majonzi au kupotelewa: kukataa, kujadili ukweli, hasira, kukata tamaa, na kukubali.

Unasihi kuhusu kifo na kufiwa unaweza kutusababishia wasiwasi kwa sababu ya hofu zetu wenyewe kuhusu kifo, au majonzi kwa ajili ya mtu fulani tuliyempenda akifariki. Kufanya unasihi wenye ufanisi tunahitaji kushughulikia hofu na hisia zetu wenyewe, ili tuweze kuwa makini kwa wateja wetu na si kuudhika tunapokuwa tunafanya kazi hiyo.

### *Kuwanasihi watoto kuhusu kifo cha watu wengine*

Mara nyingine walezi huweka kifo kuwa siri kwa mtoto. Lakini, utafiti umeonesha kwamba ni bora zaidi watoto wasikie kuhusu kifo cha mtu fulani wa karibu kutoka kwa mtu mwingine ambaye wanamwamini. Iwapo hawaambiwi, na wakasikia kutoka kwa mtu mwingine kwa bahati mbaya, wanaweza kupoteza imani, na kusikia hasira kuhusu mlezi, kutokana na kufichwa taarifa hiyo.

> Kipindi 10 ni rasilimali ya manufaa; kina taarifa na mazoezi kuhusu uelewa wa kifo, mzunguko wa uhai, na kuhimili kifo.

Watoto wa umri wa chini ya miaka mitano wanaweza kufikiri kwamba kifo kinaweza kurudishwa nyuma. Wakati tunafanya kazi nao tunahitaji kutumia hadithi na maelezo mepesi. Kwa mfano, kwanza chunguzeni pamoja iwapo mdudu aliyekufa

anaweza kutembea, kula, kuona, kupumua, na kadhalika. Kisha unaweza kueleza kwamba mdudu huyo kamwe hatafanya vitu hivyo tena, kwa sababu amekufa: hawezi tena kurudi kwenye uhai. Unaweza kuufanya ukweli huu uwe na huzuni kidogo kwa kueleza mzunguko wa maisha: kwamba watoto wa mdudu huyo wapo hai; au kwamba mdudu huyo anakuwa mbolea kwa ajili ya mimea mingine kukua, na kwa ajili ya chakula na lishe ya wadudu wengine.

Watoto wa umri wa kati ya miaka mitano hadi 10 wanao uwezekano wa kujua kwamba kifo hakibadiliki. Wanaweza pia wasielewe kwamba hakikwepeki na kwamba kinatokea kwa kila kiumbe hai. Lakini, huwa wanajaribu kuweka kizuizi kwenye kifo chao wenyewe. Ukilinganisha na watoto wadogo zaidi, wana uwezekano wa kutambua zaidi, na kuathiriwa, na uwezekano au kujua ukweli wa kifo cha mtu fulani wanayemjali.

Watoto walio zaidi ya umri wa miaka kumi hutokea kuelewa taarfa za muda mrefu za kifo na ukweli unaohusiana na kifo. Wanakuwa na uzoefu wa hisia ambao unafanana na ule wa watu wazima, lakini wanaweza kuona ugumu kuuonesha.

Kwa umri wowote ule wa mtoto, tunaweza kuwahimiza:

- ku kuwahamasisha ku eleza hisia zao kupitia michoro, michezo, simulizi za hadithi, kuandika, na kaongea;
- kuwapatia msaada katika kukabiliana na hasira zao, kujihukumu, hofu, na masikitiko;
- kuwahakikishia tena kwamba mapokeo yao hayo ni mambo ya kawaida;
- kuleta picha au kumbukumbu fulani katika kipindi cha unasihi, ili kumleta mtu huyo ambabaye amefariki kama alama ya kuwepo kwake katika kipindi;
- kuongea kuhusu mtu huyo aliyefariki kwa kushirikishana kumbukumbu za furaha na kutafakari namna ya kuhifadhi kumbukumbu za mtu huyo hai;
- kuwahamasisha watoto na walezi kutengeneza kitabu au sanduku la kumbukumbu, lenye vitu vya kusaidia kumkumbuka mtu huyo anayekufa au ambaye amefariki;
- kuchunguza kumbukumbu zozote zinazo watatiza (kwani watu mara kadhaa hukwama kwenye tukio fulani kuhusiana na ugonjwa wa mtu au kifo) na wasaidie kupata mantiki kwa mtazamo mpana;
- kufikiria kuhusu ni nani ana wapa msaada, na namna ya kuendelea na maisha yao.

Tunaweza pia kueleza kwa walezi kwamba wakati watoto wanataka kuongea kuhusu kifo, ni vizuri tukatoa mwitikio kwao. Wasaidie walezi katika kueleza watoto hali halisi, na kuwa na umakini katika mahitaji yao.

> Katika Zoezi 11.6 watoto wanatambua tarehe maalum za kuwakumbuka watu waliofariki.
>
> Tumia lile zoezi la mchezo-fumbo katika Zoezi 2.6 ili kumsaidia mtoto achukue vile vipande vilivyotapakaa vya kumbukumbu zinazomtatiza na kuvifanya viwe kitu kizima, picha chanya.
>
> Katika Zoezi 10.5 watoto wanaandaa vikuku ambamo kila kiunzi kinawakilisha mtu fulani anayewajali.

***Kumnasihi mtoto kuhusu kifo chake yeye mwenyewe***

Watoto wanaweza kuwa na hofu kuhusu uwezekano wa kifo chao wao wenyewe, hata kama sio wagonjwa. Hii inawezekana hasa iwapo wanamjua mtoto ambaye amefariki. Katika unasihi tunaweza:

- kuwasaidia watoto waongee kuhusu hofu zao, na kuwahakikishia tena kwamba ni watu wengi huhofu kuhusu kifo;
- wasaidie kukielewa kifo kama ukweli kwenye maisha, na sehemu ya mzunguko katika maisha;

- tafuta kujua imani zao za dini, na namna ambavyo zinakaa katika hali ya mtoto  ya uharaka na msaada;
- eleza kwamba hatuna usimamizi wa jumla wa afya zetu, lakini kwamba matendo yetu (kwa mfano; kumeza dawa kwa usahihi) hutoa msukumo mkubwa kwenye jambo hili;
- wasaidie kufikiria ni nini wanaweza kufanya ili kuongeza uwezekano wa kuwa na afya nzuri, na katika kufikiria kuhusu namna wanavyoishi maisha yao.

Unaweza pia kuhitaji kutoa msaada kwa watoto walio katika hatua ya mwisho ya UKIMWI. Hapa ni baadhi ya mambo kuhusu kufanyakazi na hali kama hizo.

- Fanya kazi na walezi na watu wengine ili kuongeza kujenga mazingira yenye upendo, kwa kutumia kwa mfano;  muziki ambao mtoto anaupenda; mguso muafaka kama vile kumtomasa-tomasa mikono na miguu, maua yenye harufu nzuri, makaka ya viumbe bahari au mawe; ladha anayoipenda mtoto; na uwepo wa watu ambao mtoto anawapenda;
- Wasaidie walezi kuhimili hali iliyopo, na katika kuikubali kwamba mtoto atafariki. Eleza kwamba kukubali kwao kutarahisisha kufariki kwa mtoto kwa amani, pale muda unapowadia.
- Iwapo mtoto anataka kuongea kuhusu kifo chake kinachokaribia, mhamasishe afanye hivyo.
- Uyajibu kwa uwazi na uaminifu maswali kuhusu kufa. Iwapo mtoto anauliza  'Je mimi nitakufa?',unaweza kumrudishia swali hilo kwa kusema 'Umeniuliza kama utakufa; wewe unafikiri nini? Je kifo kinamaanisha nini kwako?'
- Mahamasishe mtoto aongee kuhusu hofu zake na toa mwitikio muafaka.
- Mruhusu aeleze masikitiko yake, hasira; usijaribu kumtia matumaini.
- Mwache mtoto aongee kuhusu anavyotaka akumbukwe, iwapo anapenda.
- Usitoe maelezo kuhusu kupata nafuu; iwapo mtoto na mlezi wanadhani mtoto huyo atapata nafuu unaweza kuchunguza jambo hilo, bila makubaliano au kutofautiana nao.
- Jadilini na mtoto imani ya dini yake na, ikiwa ni muhimu, muunganishe na vyanzo vya msaada wa kiimani.

## Maneno ya kuhitimisha

Tunatumaini kwamba mwongozo huu ni wenye msaada kwako katika kazi yako muhimu. Inaweza kuwa vigumu kutenda kazi yetu vema pale ambapo kuna wateja wengi na hakuna muda wa kutosha, na iwapo hadithi zao zinatugusa na tunajiona hatuna uwezo dhidi ya changamoto wanazo kabilana nazo.  Lakini tunafahamu kwamba unasihi bora kwa hakika unawasaidia watu wazima na watoto. Tunatumaini kwamba utakatuwa na ujasiri wa kujenga stadi zako za kuwanasihi watoto na walezi wao, na utafanya kazi na wenzako ili kukuza viwango kwa ajili ya watoto hao na jamii zao.

## Vyanzo vya taarifa

Human Sciences Research Council (2012) *Legal, Ethical and Counselling Issues Related to HIV Testing of Children*; *HIV Counselling and Testing of Children: Implementation Guidelines*, Msunduzi, South Africa: HSRC <http://www.hsrc.ac.za/uploads/pageContent/3181/HIVcounsellingandtestingofchildren-implementationguidelinesWEB.pdf> [accessed 14 October 2015]

Southern African AIDS Training (SAT) Programme (2003) *Guidelines for Counselling Children who are Infected with HIV or Affected by HIV and AIDS*, Harare: SAT Programme <www.k4health.org/sites/default/files/Couselling_Children.pdf> [accessed 14 October 2015]

TUSAIDIANE PASADA

Salamander Trust
TRANSFORMING THE WAY WE THINK ABOUT HIV